www.xtrapapers.com



Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili A: literature – Higher level – Paper 1
# Swahili A : littérature – Niveau supérieur – Épreuve 1
# Swahili A: literatura – Nivel superior – Prueba 1

Friday 8 May 2015 (afternoon)
Vendredi 8 mai 2015 (après-midi)
Viernes 8 de mayo de 2015 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

**Instructions to candidates**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a literary commentary on one passage only.
- The maximum mark for this examination paper is **[20 marks]**.

**Instructions destinées aux candidats**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire littéraire sur un seul des passages.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est de **[20 points]**.

**Instrucciones para los alumnos**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario literario sobre un solo pasaje.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[20 puntos]**.



2215 – 0197

© International Baccalaureate Organization 2015

International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

www.xtrapapers.com



Andika uchambuzi kuhusu kifungu **kimoja** kati ya hizi:

**1.**

Sauti …Songa karibu nikuonyeshe mandhari. Hiki ni kidimbwi tu, wala hapana kilifi. Huyu si ngwena bali ni mjusi na pumzi zake hazizimi moto. Mwili usikufanye kibibi, kisikushike kiharusi, lazima uelemeze mizani upande wako. Haki, ni silaha inayomenya kichwa kwa kichwa, jino kwa jino, na makali yake ndiyo yaletayo amani. Tamaa ni maliwaza na dawa. Jifunge mkumbuu mwenzangu kwa sababu una uwezo wa kuvuka mto huu. *(Anakurupuka)*

Nafsi: *(Analipuka)* Wewe unajihisi unaweza kushika mbingu pasi na kuanguka. Wewe ni mtupu wa hisia. Umetuandalia sahani iliyojaa hasama na chuki na kupikiana majungu. Sahani hii lazima tuisafishe; hatutavuka hadi ng’ambo yenye mambo.

Mahiri: *(Kwa dharau)* Una uso mdogo sana mbele ya watu kunishauri Mimi. Kidudumtu hapo ulipo! Angalia unavyobingirisha macho kama gololi kwenye kidimbwi cha anguti.

Nafsi: Huu ni mkutano wa hila na nguvu. Wewe mweledi mno, unajua wasiojua watu. Hebu yajibu maswali haya mawili.

Mahiri: Uliza! Lipi la kwanza?

Nafsi: Nini kingozi chembamba kimfungacho shujaa?

Mahiri: Ni usingizi.

Nafsi: Swali la pili. Nina kitanda changu cha dhahabu na nikikilalia katu siamki. Nipe jibu muhibu mahabubu.

Mahiri: Jeneza. *(Kwa hasira)* Unadhamiria nini katika mafumbo haya? Mawazo yako hayana mvi wala chuchu, huna… Unathubutu kunifanyia stihizai na kunitapikia maswali. Una akili finyu…
*(Kwa ukali na hamasa zaidi)*

Nafsi: Itahalisi vipi uwe na macho na ujitie upofu? Uwe una masikio na ujitie uziwi? Uwe na hisia na kisha ujifanye dude? Uwe na mikono miwili na usihisi? Uwe na ubongo na ukose kupima na kuamua maswala nyeti? Na zaidi ya yote uwe na kinywa na kujishona midomo? Niambie!

Mahiri: *Shut up!* Mdomo kama msala wa umma. *(Anaamrisha)* Ondokeni nyote isipokuwa yeye. *(Akimwashiria Nafsi)* Hii ni dunia ya kupakana tope. Utapata nini wewe? Mimi nimekita kama jiwe.
*(Anaangalia kando kumpuuza Nafsi)*

Nafsi: *(Kwa watu)* Muamana haupo tena. Soni zimekimbia, nyuso zenu kavu, mnatazamana kama madubwana yasiyo hisia. Jibu lenu kila siku ni “hewalla” au kunyamaza na muda unamung’unyika. Mmeshonwa midomo? Mambo huendeshwa, hayajiendeshi yenyewe bila msukumo na kuteremsha nanga chini. Msiwe madubu bubu yanayotubu bila sababu. Haya maboni hayana uoni machoni nini? Taa hatukufunzwa kuwa haachi mwibawe? Lazima tuishi leo duniani, tusingoje kuishi kesho ahera kwenye sera mpya. Nyinyi ni washiriki dau wasoshinikiza. Mnapita na kwenda tu! Maisha ya kupiga makofi, kusifu makosa na kulala njaa. Daraja limevunjika na hamtaki kujifunza kuogelea. Mnatumbua macho tu. Ninyi ni wakereketwa wasiokerwa na chochote. Mtavua bahari kwa kuogelea?
*(Wasafiri wanatoka kwa mlio wa ngoma. Mahiri na Nafsi wanaanza kufokeana)*

Mahiri: Unateta
Unabwata
Unanidogowesha wewe
Unanirushia mshale moto kwenye moyo wangu!

www.xtrapapers.com



Nafsi: Umewawekea watu mikono shingoni na kuwabinginya na ni lazima kuitutumua kamba waliyofungiwa. Usiku umestakimu mbele yao. Anayevuruga mambo ni simba, swara anasingiziwa tu. Umeutoboa mvule wa umma. Duduvule mtoboa mvule.

Mahiri: Keki shati uipake *butter* wala sio kuila kavukavu. Mitambo ni lazima ipakwe girisi. Wahitaji kutembea sawasawa wala sio kujikongoja kiguru-cheche. Waulize waamba ngoma, wanajua wanakovutia. Wameshamchagua nguruwe na udelele unawatoka ovyo.

Nafsi: Fisi wanaotembea sawasawa na wenye unyemela unawatuma kuwasilisha nyama kwa abiria. Mmelambatia dunia tamu na kuifyonza kama kokwa ya fuu. Kufyonza damu kama kokwa ya fuu…

Humphrey N Omwaka, *Safari* (2004)

www.xtrapapers.com



**2.**

**Maombolezi ya mtu maskini**

Panya wa uhitaji naiguguna tumboni
Na kunikeketa kama msumeno
Simba wa ubepari anipachika makucha
Nakunitia mashimo mifukoni
Nami nabakia kutangatanga
Na kupepesuka kama utete tufanini.

Tanuu ya jua imeikaanga ardhi yangu
Jabali la udongo limelibutisha jembe langu
Na matiti ya uwingu wenye ubahili
Yameninyima maziwa ya kuinywesha ardhi yangu–
Ardhi ya riziki, riziki ya maisha.

Radi ya maisha imeuangukia mti wa nasaba yangu,
Na kuung'oa hadi mizizini
Mishale ya upofu imenifuma macho yangu,
Na barafu ya umri imegandia kichwani pangu;
Sina kimbilio sina tegemeo,
Sina hisi yoyote ya faraja upeoni!

Shubiri ya ufakiri imeizimua sukari yangu ya maisha,
Na miiba ya dhuluma imeitoboa mikono yangu
Nisiweze kujikimu;
Maradhi yamezidi dawa,
Na funza wa shutuma amenitekenya nyayo zangu
Nisiweze kusonga mbele.

Nimekuwa mtumwa katika dunia huru–
Fakiri katika jumuiya tajiri;
Nachungwa na kuswagwaswagwa
Kama sarakasi katika uzi!

Kwa nini? Najiuliza.
Kwa nini nasumbuka hivi, kwa nini nateseka hivi?
Natangatanga, nadidimia, nageuka kiguu na njia?
Sijui
Labda nilikufa kabla ya kuzaliwa,
Na sasa naishi baada ya kufa,
Katika enzi zisizo zangu,
Katika nchi isiyo yangu!

Labda siishi ila nadumu,
Kama kitu tu, kama kijiwe tu, kama kijitu tu!
Labda haipo siku ya wokovu abadan!
Lakini hilo si kweli, najua;

www.xtrapapers.com



Siku ya wokovu ipo,
Siku ya kukombolewa inakuja!
Itafika!
Dunia itapinduka,
Mambo yatasawazika, mtu atakuwa mtu,
Hekima itang’aa,
Miungu ya ukabaila itakufa
Na mwanadamu atakuwa huru,
Makanisa ya udhalimu yatabomoka,
Na misahafu ya ubepari itafutika.

Naam
Itakuwa siku ya makubwa,
Siku ya kitimbanga kuanguka,
Na chamchela kucharuka
Siku ya watu kufunzwa utu,
Na makabwela kupanda machela,
Siku ya mwanasiasa kushika jembe,
Na daktari kushika koleo
Ya karani kushinda mekoni,
Na afisa Kukokota troli:
Siku ya ufunuo na ufufuo!
Na siku hiyo itakapofika,
Sote tutaacha kudumu na kuanza kuishi,
Na kila mtu ataishi,
Na bunduki begani, jembe mkononi na kitabu mfukoni.

Ruo Kimani Ruo, *Nguzo za ushairi wa Kiswahili* (1989)